



AZIMIO NA. 03/2018

AZIMIO LA BUNGE LA KUMPONGEZA MHESHIMIWA DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KWA UAMUZI WAKE WA KUENDELEZA MJI WA DODOMA NA KUUPA HADHI YA JIJI

KWA KUWA, tangu aingie madarakani, Rais wa Serikali ya Awamu ya Tano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli amefanya mambo makubwa ya kuendeleza Mkoa wa Dodoma, miongoni mwa mambo aliyoyafanya ni pamoja na uamuzi wake wa kuhamisha shughuli za Serikali kuja hapa Makao Makuu Dodoma, yeye mwenyewe kuonyesha dhamira ya kuhamia Dodoma pamoja na kuutangaza Mji wa Dodoma kuwa Jiji tukio alilolifanya siku ya Sherehe za Muungano tarehe 26 Aprili, 2018;

KWA KUWA, mambo haya makubwa aliyoyafanya kwa Mkoa wa Dodoma yameleta hamasa kwa Wananchi na mwamko mkubwa wa uendelezaji wa Mkoa wa Dodoma ikiwemo ongezeko la Idara na Taasisi za Serikali kuhamia rasmi Dodoma na baadhi ya Balozi na Taasisi za Kimataifa kuonyesha nia ya kujenga na kuhamia Dodoma. Aidha, kutokana na hilo Wananchi wengi wamehamasika na kuanza kujenga nyumba bora za makazi, uwekezaji katika huduma mbalimbali za jamii umeongezeka, Serikali imeanza ujenzi wa miundombinu mbalimbali kwa mfano

kupanua Uwanja wa Ndege wa Dodoma, ujenzi wa barabara ya kuzunguka Jiji la Dodoma, ujenzi wa Mji wa Kiserikali katika eneo la Ihumwa n.k;

NA KWA KUWA, Kitendo cha kuupa Mji wa Dodoma hadhi ya Jiji kitaleta manufaa makubwa, kwani hata mgawanyo wa rasilimali (*Resource allocation*) utaongezeka ili kukidhi uendelezaji na uendeshaji wa huduma mbalimbali za kijamii zinazoendana na hadhi ya Jiji kama vile upatikanaji wa viwanja vilivyopimwa, maji safi na taka, huduma bora za afya na miundombinu imara ya barabara;

NA KWA KUWA, pamoja na kwamba mchakato wa kisheria wa kurasimisha tamko la Mhe. Rais unaendelea, maamuzi yake aliyoyafanya yamepokelewa kwa hamasa na shukrani kubwa na Wananchi wa Dodoma kwa ujumla, Wawakilishi wa Wananchi na Viongozi mbalimbali wa Mkoa pamoja na Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

KWA HIYO BASI, Bunge hili katika Mkutano wake wa Kumi na Moja, Kikao cha Hamsini, tarehe 13 Juni, 2018, linaazimia kwa kauli moja kama ifuatavyo:-

- (i) Kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumuunga mkono kwa uamuzi wake wa kuifanya Dodoma kuwa Jiji na hivyo kuliandaa Jiji la Dodoma kuendana na hadhi ya Makao Makuu ya Serikali;
- (ii) Kuiomba Serikali kuongeza rasilimali fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali itakayoendana na hadhi ya Makao Makuu na Jiji kama vile ujenzi wa barabara zenye

kiwango, miundombinu ya maji safi na maji taka, upimaji na upangaji mzuri wa Jiji la Dodoma; na

- (iii) Kuitaka Serikali ikamilishe haraka mchakato wa kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu na ikiwezekana Muswada huo usomwe Mara ya Kwanza katika Mkutano huu wa Kumi na Moja wa Bunge unaoendelea.

Limepitishwa na Bunge leo tarehe 13 Juni, 2018

Stephen Kagaigai
KATIBU WA BUNGE